

HALMASHAURI YA WILAYA YA NKASI

SHULE YA SEKONDARI MTENGA,

S. L. P. 40,

NAMANYERE-NKASI.

Mob Phone: 0785050826/0756062099

JINA LA MWANAFUNZI.....

S.L.P

NAMANYERE-NKASI

**YAH: MAAGIZO YA KUJIUNGA NA SHULE YA SEKONDARI MTENGA WILAYA
YA NKASI MKOA WA RUKWA MWAKA WA MASOMO 2021.**

1. UTANGULIZI

Ninayo furaha kukufahamisha kuwa umechaguliwa kujiunga na kidato cha kwanza katika shule ya Sekondari Mtenga kwa mwaka wa masomo 2021, shule ipo km 20 kutoka makao makuu ya wilaya ya Nkasi-Namanyere.

Muhula ya kwanza wa masomo unaanza tarehe 11/01/2021 hivyo unatakiwa kuripoti hapa shuleni Jumatatu ya tarehe 11/01/2021 saa 1:00 asubuhi.

Mwisho wa kuripoti mwanafunzi wa kidato cha kwanza ni tarehe 15/01/2021. Baada ya hapo mwanafunzi hatapokelewa na nasafi yake itafutwa na mzazi au mlezi atachukuliwa hatua kali za kisheria.

2. MAMBO MUHIMU YA KUZINGATIA

➤ SARE YA SHULE

a) SARE YA SHULE KWA WAVULANA

- i. Mashati mawili (2) rangi nyeupe ya tetroni mikono mifupi
- ii. Suruali mbili (2); Moja ya rangi ya kijani, ya pili rangi nyekundu damu ya mzee zenye rinda.
- iii. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi vyenye kamba
- iv. Sweta rangi ya kijani, nyeusi kwa ajili ya baridi.
- v. Soksi zaidi ya pea mbili rangi nyeusi.

b) SARAE YA SHULE KWA WASICHANA

- i. Mashati mawili (2) rangi nyeupe ya tetroni mikono mifupi.
- ii. Sketi mbili (2), moja ya rangi ya kijani, na nyingine rangi nyekundu damu mzee ndefu inayofika kwenye fundo la mguu karibu na unyayo.
- iii. Viatu vya ngozi jozi mbili (2) rangi nyeusi vyenye kamba
- iv. Sweta rangi ya kijani, nyeusi kwa ajili ya baridi.
- v. Soksi zaidi ya pea mbili rangi nyeupe.

3. Kwa wazazi/walezi watakaopenda watoto wao wa kike walale **hostel** wanatakiwa kuwapatia mahitaji yafuatayo;

- a) Godoro dogo futi $2\frac{1}{2}$.
- b) Blanket moja
- c) Shuka moja rangi ya pinki na mto mmoja.
- d) Chandarua kimoja
- e) Gauni la bluu bahari kwa ajili ya kazi za nje.
- f) Mzazi atampatia mtoto wake chakula cha kutosha ili ajipikie mwenyewe na fedha ya matumizi. Shule itatoa stoo ya kutunzia na jengo la jiko la kupikia.

4. VIFAA VYA DARASANI

- a) Daftali kumi aina ya counter books (10) kwa ajili ya notisi na mazoezi shuleni.
- b) Kalamu na penseli za kutosha
- c) Mkoba (bag) la kubebea madaftari
- d) Mkebe (mathematical set) na rula ya sm 30
- e) Dictionary ya English – Kiswahili

5. VIFAA VINGINE

- a) Alete ndoo lita kumi ya kufanyia usafi
- b) Alete jembe jipya lenye mpini la kulimia

Pamoja na vifaa hivyo mwanafunzi anatakiwa kuzingatia yafuatayo;

- Aje na cheti cha kuzaliwa
- Bima ya afya
- Ajaze form ya **MEDICAL EXAMINATION** iliyoambatanishwa nyuma katika hospitali ya serikali


6. SHERIA NA KANUNI MUHIMU ZA SHULE

Mwanafunzi anatakiwa kuzingatia mambo ya msingi yafuatayo;

- i. Heshima kwa viongozi, wazazi, wafanyakazi wote na jamii kwa ujmla ni jambo la lazima.
- ii. Maudhurio mazuri katika shughuli ndani na nje ya shule kulingana na ratiba ya shule ni lazima
- iii. Kushiriki kwa makini maandalio ya jioni (preparation)
- iv. kuwahi katika kila shughuli za shule na nyingine utakazopangiwa.
- v. Kuvaa sare ya shule wakati wote
- vi. Kutunza usafi wa mwili, mavazi na mazingira ya shule
- vii. Kuzingatia ratiba ya shule
- viii. Kutunza mali za shule
- ix. Ni mwiko kwa mwanafunzi kutishia usalama wa mtu yeyote Yule.

7. MAKOSA YAFUATAYO YANAWEZA KUSABABISHA KUFUKUZWA SHULE;

- i. Wizi, Uasherati, ushoga na Ubakaji
- ii. Ulevi na matumizi ya madawa ya kulevya kama vile uvutaji bangi, cocaine, mirungi, kubeli na kadhalika
- iii. Kupigana au kupiga
- iv. Kuharibu kwa makusudi mali ya umma
- v. Kudharau Bendera ya taifa
- vi. Kuwa mjamzito/kupata mimba au kusababisha mimba.
- vii. Kuo au kuolewa
- viii. Kutoa mimba
- ix. Kugombana, kuchochea na kuongoza au kushiriki kuvuruga amani na usalama wa shule.
- x. Kukataa adhabu
- xi. Kuwa na simu ya mkono au laini ya simu.


R. MAHAMOUD
MKUU WA SHULE
THE HEAD MASTER
MTEENCA STD SCHOOL

MEDICAL EXAMINATION FORM.

MTENGA SECONDARY SCHOOL

P.O. BOX 40,

NKASI

DATE;.....

**MEDICAL OFFICER,
GOVERNMENT HOSPITAL.
P.O.BOX**

REQUEST FOR MEDICAL EXAMINATION.

Please examineas to his/her fitness for pursuing further education at this school.

- 1. Haemolobin
- 2. P. V Bleeding
- 3. Blood pressure
- 4. Blood group.....
- 5. (a) Sight
- (b) Hearing
- 6. Urine for sugar and pregnancy test.....
- 7. Stool for routine examination.....
- 8. Asthma
- 9. Skin disease's.....
- 10. Leprosy.....
- 11. Epilepsy.....
- 12. Pulmonary.....
- 13. Deformity.....
- 14. Mental problem.....
- 15. V. D (GVE TYPEF).....
- 16. Any other serious disease (not mentioned above).....
- 17. Cheek Pregnancy.....

COMMENT.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....
.....

DESGNATION AND SIGNATURE
.....
.....
.....
.....
.....